**CHRISTIAN SOCIAL SERVICES COMMISSION (CSSC)**
**NORTHERN ZONE JOINT EXAMINATIONS SYNDICATE (NZ-JES)**

**FORM FOUR PRE – NATIONAL EXAMINATION AUG 2025**

**0015** **ELIMU YA DINI YA KIISLAMU**

MARKING SCHEMES

1.MAJIBU

| i | Ii | Iii | Iv | v | vi | vii | viii | Ix | X |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| A | C | D | D | D | C | D | B | B | D |

2.MAJIBU

| ORODHA A | I | ii | iii | iv | v | vi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| ORODHA B | E | B | G | H | C | D |

SEHEMU B MAJIBU

3. Katika jamii yako kuna matendo mengi yanafanywa yanayokwenda kinyume na haki na uadilifu na watu hao wanadai kuwa ni vigumu kuishi kwa kutenda haki kutokana na mazingira. Tumia hoja tatu kuwaonesha kuwa inawezekana jamii hiyo kuondokana na hali hiyo mbaya. (**Alama 9 @ 3)**

**JIBU**. Katika hali yoyote ile katika jamii, haki na uadilifu unaweza kutekelezwa ikiwa watu wake watasifika na hali tatu zifuatazo:

(i) Kushikamana na Tawhiid: Jamii inaposhikamana na kumpwekesha Allah ipasavyo daima watakuwa watekelezaji wa haki na uadilifu, kwani waja wakishikamana na shirki daima watazama katika kudhulumiana na kufanyiana mengine mengi, na anayemdhulumu Allah katika ibada yake ni rahisi Zaidi kumdhulumu mwenzie.

(ii) Kushikamana na risala (Utume/Ujumbe): Suala la haki na uadilifu ni katika sheria za Allah, na Allah hufikisha sheria zake kwa waja wake kupitia Mitume (ujumbe), hivyo jamii ikizingatia ujumbe ulioletwa na Mitume wa Allah daima watakuwa watekelezaji wa sera ya Allah ya haki na uadilifu.

(iii) Kuwa na Imani juu ya siku ya mwisho: Jamii inapoamini kuwa ipo siku waja wataulizwa na kuhukumiwa kutokana na matendo yao watajizatiti katia kutenda mema kwa watu na kutowafanyia dhulma yoyote ile wasiende kulipa madeni siku ya hukumu. Kwa kufanya hivyo haki na uadilifu katika jamii hiyo itasimama

4. Wanafunzi wa kidato cha tatu wanatamani kujua historia ya Maswahaba baada ya kutawafu Mtume (Sallallahu Alayhi Wasallam) hasa katika kipengele cha kuporomoka kwa Dola ya Kiislamu. Tumia hoja tatu kuwafahamisha sababu zilizopelekea jambo hili baya kutokea.(**Alama 9@ 3)**

**JIBU**.Kudondoka kwa Dola ya Kiislamu aliyoiacha Mtume Muhammad (s.a.w) kumesababishwa na mambo mbalimbali, miongoni mwa mamb hayo ni:

(i)Fitna za Abdullah bin Sabai: Hii ndio ilikuwa sababu kuu, kwani kutokana na hili yafuatayo yalitokea:

- Kuuawa kwa Khalifa Uthman (Khalifa wa tatu)
- Vita vya Waislamu kwa Waislamu (Ngamia na Siffin)
- Kuuawa kwa Khalifa wa nne (Ali)

(ii) Migogoro ya kisiasa: Hii ilisababisha uongozi wa Ki-Khalifa utoweke na kuanza kwa uongozi wa Kifalme (Ukoo). Mfano dola ya Umaiyah iliyoongozwa na watu kutoka ukoo wa Umaiyah na Dola ya Ubbasiy na nyinginezo. Kubomoka kwa Shura iliyoachwa na Mtume (s.a.w).

5. Katika kongamano la wazazi Sheikh Mundele alitakiwa kuwasilisha mada ya malezi ya Watoto kimaadili. Bainisha dondoo tatu atakazoweza kuzitumia Sheikh huyu katika kufikisha mada yake hii. **(Alama 9 @ 3)**

**JIBU.**Malezi ya Watoto kimaadili.

(i) Kumuadhinia

Kuna hekima nyingi katika kufanya hivi, miongoni mwake ni kuna dua kwa mtoto awe mja mwema mwenye kusimamisha swala, na kusimamisha Uislamu katika jamii.

(ii) Kumfanyia mtoto Aqiqah

Katika Aqiqah mtoto mwanaume anachinjiwa mbuzi au kondoo wawili na kwa mwanamke mmoja, hii inakuwa katika siku ya saba ya kuzaliwa kwa mtoto. Hekima ya kumfanyia mtoto Aqiqah ni mzazi kumshukuru Allah kwa neema ya kizazi, na kumuombea mtoto ulinzi kutoka kwa Allah amchunge kila baya na amfanye mja mwema.

(iii)Kumpenda na kumhurumia mtoto

Wazazi wanatakiwa kuwa na upendo na Watoto na kuwahurumia kwa kuwafanyia Watoto hao mambo wanayoyapenda madam ni halali. Watoto wanapokosea warekebishwe kwa sauti ya wastani, ukali uliopindukia unaweza kumuweka mtoto mbali na mzazi kiasi atashindwa kueleza changamoto zake kwa mzazi wake.

Hoja nyingine ni pamoja na: Kuwaelimisha Watoto Kuwapa Watoto nasaha

6. Mkataba wa Hudaybiyah una mafunzo mengi ya namna ya kuishi na wasio Waislamu huku unatekeleza jukumu la kusimamisha Uislamu katika jamii yako. Thibitisha kauli hii kwa kubainisha mafunzo sita (6) kutoka kwenye mkataba huo. **(Alama 9 @ 1.5)**

   **JIBU**. Mafunzo ya Mkataba wa Hudaybiyah katika namna ya kuishi na wasio Waislamu huku unaendelea na jukumu la kusimamisha Uislamu katika jamii.

   (i) Katika mchakato wa kusimamisha Uislamu ni lazima kuwepo mbinu na mipango ya muda mrefu na muda mfupi ili malengo yanayokusudiwa yafikiwe.

   (ii) Katika Uislamu ni wajibu kwa Waislamu kutekeleza mikataba waliowekeana hata ikiwa na makafiri kama alivyofanya Mtume (Sallallahu Alayhi Wasallam) katika mkataba huu.

   (iii) Ni wajibu kuwafikishia ujumbe wa Uislamu wasio Waislamu na viongozi wao kwa kutuma mabalozi na njia nyingine zinazofaa.

   (iv) Mazingira ya amani ni muhimu sana katika mchakato wa kusimamisha Uislamu, hivyo ni bora zaidi kuitafuta kwa gharama yoyote, na inapokuwepo ni wajibu kuilinda.

   (v) Waislamu wanapaswa kuwa wepesi wa kutumia fursa pindi inapopatikana hata kwa uchache, ili kjfikia malengo ya kusimamisha Uislamu katika jamii.

   Waislamu wanapaswa kuwa tayari kuacha maslahi muhimu ili kupata maslahi muhimu zaidi kwa makusudio ya kufikia malengo makuu

7. Umar bin Abdul-Aziz anachukuliwa kama Khalifa wa tano wa Uislamu kutokana na namna alivyokuwa anasimamia mambo ya Dola katika uongozi wake. Ni mambo gani sita wanaweza kujifunza viongozi wa sasa ili jamii zao ziishi kwa amani, upendo na uadilifu? **(Alama 9 @ 1.5)**

   **JIBU**. Mambo wanayoweza kujifunza viongozi wa sasa kutoka kwa kiongozi Umar bin AbdulAzizi.

   (iii) Kuhakikisha fedha za uma zinazokusanywa kwa uadilifu na kutunzwa kwa ajili ya manufaa ya watu wote.

   (iv) Kutengua uongozi wa viongozi ambao wanaongoza raia kikaili.

   (iii) Maafisa wanaotumia vibaya mali za uma kuchukuliwa hatua kali.

   (iv) Kuhakikisha kuwa vipimo na mizani vinasimamiwa kwa haki.

   (v) Viongozi kuwa karibu na raia kwa kutenga muda wa kusikiliza changamoto mbalimbali walizonazo na kuzifanyia kazi.

   (vi) Kuhakikisha raia wote wanapata haki sawa katika kumiliki rasilimali za nchi, kama ardhi n,k.

   (vii) Kutenda haki kwa raia wote bila ya kujali dini au hali ya mtu.

   (viii) Kusikiliza maoni mbalimbali ya watu katika kuendesha nchi.

   (ix) Ukusanyaji wa kodi uzingatie kipato cha mtu na usiwe mzigo kwa raia.

   (x) Kupiga marufuku mishikamano ya kikabila na watu waishi kama wamoja.

8. Mtaani kwenu kumetokea watu wanaoeneza itikadi mbaya ya kwamba kuna Mtume mwingine atakayekuja baada ya Mtume Muhammad (Sallallahu Alahyi Wasallam). Hoja gani tatu utakazotumia kufuta itikadi hii potofu ili watu wasipotee?

**JIBU**.Hoja zinazoonesha kuwa Hapana Mtume mwingine baada ya Mtume Muhammad (Sallallahu Alayhi Wasallam).**(Alama 9 @ 3)**

(i) Mafundisho aliyokuja nayo Mtume Muhammad (Sallallahu Alayhi Wassalaam) yapo hai na yamehifadhiwa kwa ahadi ya Allah.

Allah Mtukufu ameahidi kulinda ujumbe wa Qur'an kutokana na kuharibwa kwa namna yoyote ile, ili mwongozo anaoutaka ufike kwa wahusika wote bila ya kasoro. Si hivyo tu, bali hata mafundisho ya Mtume (Sunnah) yamehifadhiwa aktika hadithi sahihi zilizokidhi vigezo vyote. (Isnad na matini). Hivyo kwa hoja hii sharti la kuletwa Mtume mwingine limeondoka.

(ii) Allah ameukamilisha mwongozo wake kwa Mtume Muhammad (Sallallahu Alayhi Wasalaam) na hivyo kuufanya Uislamu kuwa mfumo wa Maisha uliokamilika pasi na kasoro. Qur'an (5:3). Kwa hoja hii hitajio la Mtume linaondoka.

(iii) Mtume Muhammad (Sallallahu Alayhi Wasallam) ameletwa kwa ajili ya watu wote na wala hakuletwa kwa ajili ya watu Fulani tu kama ilivyokuwa kwa Mitume waliomtangulia.

Qur'an inasema; "Sema (Ewe Nabii Muhammad) Enyi watu! Hakika mimi ni Mtume wa Allah kwenu nyinyi nyote …." (7:158)

Aya hii na nyingine nyingi zinaonesha kuwa Hapana haja tena ya kuletwa Mtume mwingine baada ya huyu wa mwisho.

SEHEMU C MAJIBU

9. Katika hukumu za Kiislamu baada ya Qur'an kigezo kinachofuata ni Hadith sahihi za Mtume Muhammad (Sallalahu Alayhi Wasallam). Wabainishie watu wa Msikitini kwako sifa tano zinazoitofautisha na aina nyingine za kigezo cha usahihi ili watu waweze kufanyia kazi mafundisho yaliyo sahihi tu.

**Utangulizi Alama 1**
**Point alama 1 (1 x 5 )**
**Maelezo 2 (1.5 x 5)**
**Hitimisho 1**

**JIBU**.Sifa za Hadithi sahihi za Mtume Muhammad (Sallahu Alayhi Wassallam).

(i) Pawepo na muungano wa wapokezi wa Hadith, Mpokezi awe amepokea moja kwa moja kwa yule aliyeko juu yake kutoka mwanzo wa Isnad mpaka mwisho wake. Kwa maana nyingine ni kwamba Isnad isiwe na mapengo.

(ii) Uadilifu wa mpokezi; kila mpokezi wa Hadith awe ni Muislamu, baleghe, mwenye akili asiwe fasiki na mwenye kufanya mambo ya hovyo.

(iii) Udhibitifu wa Mpokezi; Ni kuwa kila mpokezi wa aina hii ya Hadithi anatakiwa awe vizuri katika kuhifadhi ima kifuani au katika maandishi (kuandika) udhaifu katika sifa hii huitoa Hadithi katika Daraja la usahihi.

(iv) Kutokwenda kinyume na aliyekuwa mdhibitifu zaidi. Mpokeaji asitofautiane (kukhalifiana) na yule anayejulikana kuwa ni mzuri zaidi katika kudhibiti mambo, kwani kutokea kwa hali hiyo huweza pelekea shaka juu ya Hadithi husika na kuifanya itoke katika Daraja la usahihi.

(v) Kutokuwa na kasoro (ila); Hadithi sahihi haipaswi kuwa na kasoro yoyote iliyojificha inayoweza kusababisha kutokusihi kwake, hata kama muonekano wake wa nje hauoneshi wasiwasi wowote.

10. Japokuwa Qur’an yote imetoka kwa Allah, lakini pana tofauti kati ya sura za Qur’an zilizoshuka Makkah na zile za Madinah.Tumia hoja **tano** kuonesha hali hiyo.
JIBU. Tofauti kati ya Sura za Makkah na Madinah

| SURA ZA MAKKAT | SURA ZA MADINA |
|---|---|
|  **Walengwa**: Sura hizi zimeshushwa Makkah katika kipindi cha mwanzo wa Utume. Hivyo zilizingatia mazingira ya jamii ya Waarabu kwa ujumla ambao walizama kwenye ushirikina. Pia aya za Makka ziliwalenga Waumini wa mwanzo. | **Walengwa**:. Sura ziliwalenga Waumini ambao wanapaswa kusimamisha Dola ya Kiislamu na kuiendeleza. Kwa upande mwingine Sura za Madina ziliwalenga maadui wa Dola ya Kiislamu miongoni mwao ni wanafiki na washirikina. |
|  **Ujumbe**: Katika kipindi cha Makka ujumbe wa Qur’an kwa kiasi kikubwa ulijihusisha na ujenzi wa imani ya kweli juu ya Mwenyezi Mungu, Malaika wake, Vitabu vyake, Mitume wake, siku ya mwisho na Qadar yake. | **Ujumbe:** Ujumbe wa Qur’an kwa kiasi kikubwa ulijihusisha na ujenzi wa jamii ya Kiislamu, usimamishaji, uendeshaji na ulinzi wa Dola ya Kiislamu. Pia vipengele vya sharia mbalimbali vinaainishwa, pamoja na hukumu za mambo mbalimbali. |

| | |
|---|---|
|  **Muundo wa Sura**: Takriban sura zote za Makka zina aya fupi fupi zenye kufikia lengo moja. Vile vile nyingi ya sura hizi ni fupi. | **Muundo wa sura:** Takriban sura za Madina nyingi zimejengwa na aya ndefu ndefu zilizoundwa kwa kutumia lugha ya kisheria, inayofafanua masuala mbalimbali na kuyaweka bayana kiutekelezaji. Vilevile nyingi ya sura hizi ni ndefu. |
|  **Mbinu**: Hapa imetumika lugha ya mchomo inayogonga moja kwa moja kwenye moyo wa mlengwa. Allah ameapia maumbile mbalimbali ili yawe ushahidi ulio wazi juu ya ujumbe uliofikishwa. Pia Allah ametumia historia ya watu waliopita ili kuwakhofisha na kuwakatisha tamaa wapinzani wa ujumbe wa Allah kwa upande mmoja na kwa upande wa pili kuwaliwaza na kuwatia moyo na hima wasimamizi na watekelezaji wa ujumbe wa Allah. | **Mbinu**: Hapa imetumika lugha ya sheria au lugha ya ufafanuzi ili kuwawezesha waumini kuutekeleza Uislamu vilivyo katika kila kipengele cha maisha. Pia Allah ametumia historia ya Mitume waliotangulia ili kwa upande mmoja kuwakatisha tamaa wapinzani wa dola ya Kiislamu na kwa upande mwingine kuwapa waumini moyo wa matumaini kuwa wakijizatiti katika kupigania Dini ya Allah watashinda na watakuwa juu ya makafiri, washirikina na wanafiki kwa hali yoyote iwayo. |

11. Chambua madhara matano ya kutofikiwa kwa lengo la ibada ya Zakat katika jamii ya Waislamu wa Kigoma.

**Utangulizi Alama 1**
**Point alama 1 (1 x 5 )**
**Maelezo 2 (1.5 x 5)**
**Hitimisho 1**

**JIBU**. Madhara ya kutofikiwa kwa lengo la zakat katika jamii.

(i) Kukosekana kwa uadilifu katika uchumi wa jamii.

(ii) Kukosekana kwa upendo na huruma baina ya wanadamu.

(iii) Kuongezeka kwa kundi wasiyo jiweza na tegemezi katika jamii.

(iv) Kuporomoka kwa uchumi wa jamii.

(v) Kuenea kwa riba na madhara yake.

(vi) Kuporomoka kwa maadili ya kijamii.